# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema pamoja na kutuwezesha kufika katika Baraza hii leo ili kuendelea kutekeleza majukumu ya kujenga nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake imara uliojaa hekima na busara na wenye azma kubwa ya kuiletea Zanzibar maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa na kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa jitihada zao wanazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri Baraza letu la Wawakilishi. Vile vile, ninawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza, kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu, umakini na uweledi. Kamati hizi zimeweza kutoa ushauri na maelekezo yanaosaidia sana utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026

.

**Mheshimiwa Spika**,

Naomba nichukue nafasi hii niwashukuru watendaji kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Wizara ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Omar Said Shaaban kijana ambae tunaamini Mheshimiwa Raisi alimpa nafasi hii kwa kutambua uwezo wake na umahiri wake katika kazi. Hivyo, pamoja na uwezo na ueledi wa Mheshimiwa Waziri tunamuomba asiache kuifuata miongozo iliyowekwa ili Nchi yetu iweze kufunguka katika sekta ya Biashara na Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**,

Naomba nitumie fursa hii, kumpongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada wanazozichukuwa katika kuiletea nchi yetu maendeleo na mabadiliko chanya katika sekta hii ya Biashara.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba pia kutumia nafasi hii kuwashukuru Wafanyabiashara wote, Taasisi binafsi, pamoja na wawekezaji wa viwanda nchini ambao ndio wadau wakubwa katika sekta hii ya Biashara na Viawanda.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kutekeleza majukumu yao vyema na naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo.

| | |
|---|---|
| Mhe. Mtumwa Pea Yussuf | Mwenyekiti |
| Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Makamo Mwenyekiti |
| Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Mjumbe |
| Mhe. Mihayo Juma Suleiman | Mjumbe |
| Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| Mhe. Dk Mohammed Ali Suleiman | Mjumbe |
| Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii inafanya kazi zake kwa karibu sana na makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

| | |
|---|---|
| Ndg Asma Ali Kassim | Katibu |
| Ngd Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| Ndg Abubakar Mahmoud Iddi | Katibu |
| Ndg Azmina Khamis Hamad | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilipitisha bajeti ya Wizara ya Bisahara na Maendeleo ya Viwanda kwa kuangalia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais katika kampeni zake katika sekta hizi pamoja na malengo yake yanayopatikana katika hotuba aliyokuja kuiwasilisha hapa Barazani wakati wa uzinduzi wa Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuanza kuelezea Programu kuu na ndogo za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 naomba kwanza nichukue fursa hii kuelezea maoni ya Kamati kuhusiana na mapato ya Wizara kwa mwaka wa 2024/2025. Kamati yetu imepata nafasi ya kupitia kwa makini makadirio yaliowalisilswa na Wizara na tulipata nafasi ya kujadiliana na kushauriana kwa lengo la kuboresha ili Wizara iweze kufanya shughuli zake kwa weledi.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilion 1.93 kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa, ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi bilioni 1.50.

**Mheshimiwa Spika,**

Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi Bilioni 1.20 zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo ni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi tisa (9). Kamati yangu inatoa pongezi zake kwa wote waliofanikisha kupatikana kwa kiwango hicho na tunaimani kwa miezi mitatu iliyobakia watakamilisha asilimia 100%.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepangiwa kukusanya jumla ya Shilingi billioni 3.51 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2024/2025 ya Shilingi bilioni 1.93. Mapato hayo yatakusanywa kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo haina pingamizi juu ya Ukusanyaji wa Mapato hayo na tuna matarajio makubwa ya kuongezeka ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha. Lakini kama tunavyojua pesa huzaa pesa, Hivyo tunaiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ijenge utaratibu wa kuwaingizia kwa wakati fedha za kuendesha Ofisi (OC) ili na wao waweze kukusanya kile walichopangiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepanga kutekeleza Programu zake kuu nne kama ifuatavyo:

i) Programu ya Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biashara;

ii) Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;

iii) Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara;

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kutekeleza  Programu hizo, bajeti ya kutosha inahitajhika ili lengo liweze kufikiwa na wananchi waweze kunufaika. Pamoja na bidii zilizochukuliwa na Serikali bado juhudi kubwa inahitajika kwa kuweka fedha za kutosha katika kila programu ili yale yalioahidiwa na Serikali yaweze kutimia.

## ROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapenda kutoa pongeza kwa Serikali kwa juhudi zake inazoendelea kuzichukua katika suala zima la uimarishaji wa viwanda pamoja na uimarishaji wa uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo. Programu hii kwa mwaka uliopita ilikadiriwa jumla ya shilingi 20,514,641,000 wakati kwa mwaka huu wa 2025/2026 programu hii imekadiriwa jumla ya shilingi 36,012,784,000.

Hata hivyo, pamoja na fedha kuongezeka katika programu hii, Kamati yangu inasisitiza

umakini na usimamizi mzuri katika kuratibu shughuli zilizopangwa ili tuone matokeo chanya kupitia huduma zinazotolewa kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuimarisha Biashara na Kutafuta Masoko nchini, Wizara imejipanga kuendeleza ujenzi kwenye eneo la Kituo cha maonesho ya kibiashara Diman na Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre). Kwa program hizi mbili tunaimani Wizara itaweze kuendeleza utaratibu wa kuhakikisha masoko yanapatikana nje na ndani ya nchi ili wafanya biashara wetu wapate kunufaika kwa kusaidiwa kupatiwa masoko ili wauze bidhaa zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa 2025/2026 programu hizi zimepangiwa makadirio ya shilingi, 17,021,117,000. Tuna imani kubwa malengo yote yaliopangwa yatakamilika , hivyo tunaiomba Wizara kuendeleza umakini katika kuratibu kazi zake ili matarajio yaliopangwa yaweze kutimia.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara yetu imepata mafanikio makubwa kwa mwaka wa fedha huu ambao tunaumaliza na kwa ruhusa yako naomba niyataje kwa ufupi kama ifuatavyo, Wizara imefanikiwa kukamilisha mfumo wa Taarifa za Viwanda (Industrial Information System) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa ajili ya kupokea taarifa za viwanda ikiwemo uzalishaji, ajira pamoja na changamoto mbali mbali za wenye viwanda.

**Mheshimiwa Spika,**

Hii ni hatua kubwa kwa Wizara na Nchi kwa ujumla kwani itarahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu zenye lengo la kuboresha na kudhibiti ajira, kujua kiwango cha uzalishaji nchini na kuchukua hatua za haraka kwa Wizara pindi itakapoona kuna jambo linahitaji maamuzi kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, Kamati yetu imebaini changamoto kadhaa ambazo zisipofanyiwa kazi kwa haraka zinaweza zikapunguza kasi ya utendaji kazi kwa Wizara, Changamoto hizo ni kama vile kutotumika kwa Sheria ya Usajili wa Amana kwa mali zinazohamishika, Uelewa mdogo wa Usajili wa Mali Bunifu kwa upande wa Wazanzibari na Uelewa mdogo wa madaraja ya karafuu kwa wakulima ni changamoto ambayo inaikabili Shirika la Biashara Zanzibar. Hivyo, elimu itolewe kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** tunaomba fedha zilizokadiriwa katika bajeti hii zipatikane kwa wakati na zipatikane kama zilivyokadiriwa**.**

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Biashara, Utalii, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao ili tuweze kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kuwasilisha.

Ahsante sana

……………………………,

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu,

M/Mwenyekiti,

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**